

## **SEKTA YA AFYA:**

### **UTANGULIZI**

Huduma za afya zilianza kutolewa kabla ya uhuru chini ya Mashirika ya Dini RC na Anglikana. Roman Catholic walikuwa na hospitali mbili (Litembo na Lituhi) na zahanati 5. Kanisa Anglikana lilikuwa na zahanati 2 na hospitali 1. Watumishi wengi walikuwa toka nje ya nchi na wachache watanzania (kada za chini) 10.

Baada ya Uhuru mwaka 1970 Serikali ilijenga kituo cha afya Mbinga Mjini na watumishi walioanzisha kituo cha afya walikuwa 18. Mwaka 1971 zilianza huduma shirikishi kati ya Serikali na Mashirika ya Dini. Watumishi waliendelea kuongezeka sambamba na vituo vya huduma. Hadi mwaka 1977 idadi ya vituo vya huduma vilikuwa 16. Mashirika ya dini vituo 12 na Serikali vine (4).

Wakati tulipopata uhuru wananchi walikuwa wakisumbuliwa zaidi na magonjwa ya malaria, pneumonia, magonjwa ya kuhara, kisonono, kaswende na magonjwa mengine ya kuambukiza. Wananchi kwa wakati huo walikuwa wakitumia huduma za waganga wa kienyeji zaidi na afya zao kwa ujumla haikuwa nzuri sana.

### **HALI YA SASA**

Hali ya utoaji wa huduma za afya katika wilaya ya mbinga imeboreka zaidi ambapo vituo vya kutolea huduma vimeongezeka hadi 88 kwa mchanganuo ufuatao;

<b>Hospitali 5</b>			<b>Vituo Vya Afya 10</b>			<b>Zahanati 73</b>		
<b>Serikali</b>	<b>Dini</b>	<b>Private</b>	<b>Serikali</b>	<b>Dini</b>	<b>Private</b>	<b>Serikali</b>	<b>Dini</b>	<b>Private</b>
1	4	0	6	4	0	59	12	2

Watumishi wameongezeka kufikia 688 wilayani na wote ni Wazalendo.

## **MAFANIKIO**

1. Vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka toka 10 kabla ya uhuru hadi 88 kwa sasa
2. Wananchi wanavitumia vituo hivi zaidi kwa huduma za magonjwa yote
3. Afya ya mazingira imeboreshwa zaidi mijini na vijijini
4. Upatikanaji wa madawa na vifaa tiba umeboreka zaidi
5. Vifo vya akinamama wajawazito vimeendelea kupungua hadi kufikia 79/100000 mwaka 2010
6. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano navyo vimepungua 23/1000
7. Huduma za afya zimesogezwa zaidi karibu na wananchi.

## **CHANGAMOTO**

1. Upatikanaji wa vifaa tiba dawa na vitendanishi toka MSD umekuwa si wa kuridhisha.
2. Vyenzo vya kazi ikiwemo magari yamekuwa si ya kutosheleza.
3. Miundombinu ya barabara imekuwa haipitiki hasa wakati wa mvua hivyo kutoweza kufikisha huduma.

## **MATARAJIO YA BAADAE**

1. Kuendelea kusogeza huduma za afya zaidi kwa kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata
  2. Kuendelea kutoa huduma za kinga ili wananchi wasiugue magonjwa yanayoambukiza
- Kuboresha huduma za tiba ili wananchi wasifariki kutokana na magonjwa yanayotibika